

Bima Mpya ya Afya kwa Watu Wazima

Kuanzia tarehe 1 Januari, 2019, watu wazima zaidi wanaoishi Virginia wanaweza kupata bima ya afya yenye ubora, ya bei nafuu na ya bila malipo!

Je, Bima Mpya ya Afya kwa Watu Wazima ni Nini?

Sheria za Medicaid zimebadilika. Hii inamaanisha kuwa ikiwa ulituma ombi la Medicaid awali na ukanyimwa, huenda sasa ukastahiki. Kuanzia tarehe 1 Novemba, 2018, watu zaidi wanaweza kustahiki bima ya afya kupitia Medicaid. Fidia zitaanza tarehe 1 Januari, 2019.

Watu wanaofanya kazi katika biashara rejareja, ujenzi, malezi ya watoto, usanifu wa bustani, huduma za vyakula na kazi nyingine nyingi wasio na bima ya afya, sasa wanaweza kustahiki.

Bima mpya ya afya kwa watu wazima inatoa fidia bora kwa familia za mapato ya chini ambazo huenda zisiweze kupata huduma ya afya.

Je, Inafidia Nini?

Bima mpya ya afya inafidia watu wazima:

- Huduma za daktari, hospitali na dharura
- Dawa za maagizo
- Huduma za maabara na Eksrei
- Huduma ya uzazi na watoto wanaozaliwa
- Utunzaji wa muda mrefu na huduma za usaidizi
- Huduma za afya nyumbani
- Huduma za afya ya tabia ikiwemo uraibu na huduma za tiba ya kupona
- Huduma za urekebishaji ikiwemo tiba za mwili, shughuli za kila siku na matamshi.
- Usafiri kuenda kwenye huduma zinazofidiwa na Medicaid wakati hakuna njia mbadala
- Huduma za uzazi wa mpango
- Vifaa vya matibabu
- Huduma za uzuiaji na ustawi na huduma za udhibiti wa ugonjwa sugu
- Na zaidi!

Je, Nani Anafidiwa?

Watu wazima wanaweza kustahiki bima mpya ya afya ikiwa:

- Wanaishi Virginia
- Wana miaka 19 – 64
- Hawapati wala kustahiki Medicare
- Wanakidhi matakwa ya mapato, yanayotofautiana kulingana na ukubwa wa familia

Kikomo cha Mapato ya Bima ya Watu Wazima (Jumla*)

Ukubwa wa Familia	Kwa Mwezi	Kwa Mwaka
1	\$1,677	\$20,121
2	\$2,268	\$27,214
3	\$2,859	\$34,307
4	\$3,450	\$41,400
5	\$4,042	\$48,494
6	\$4,633	\$55,587

*Itaanza kutumika tarehe 20 Januari, 2023. Vikomo vya mapato vinarekebishwa kila mwaka

Je, Nitatuma Vipi Ombi?

- Wasiliana na Cover Virginia Call Center kwa 833-5CALLVA. Wakalimani wanapatikana. Wawakilishi wetu watakuunganisha na mtu anayezungumza lugha unayopendelea.
- Kamilisha ombi la mtandaoni kwenye Common Help: www.commonhelp.virginia.gov
- Kamilisha ombi la mtandaoni kwenye The Health Insurance Marketplace: www.healthcare.gov
- Tuma barua au wasilisha ombi kwa njia ya karatasi kwenye Department of Social Services

Kwa orodha ya nyaraka ambazo utahitaji unapotuma ombi, tembelea www.coverva.org na ubofye ukurasa wa Tuma Ombi.